Mafunzo ya Wasaidizi Ustawi wa Jamii Awamu ya Pili:

Kuwajengea stadi za kuwashughulikia watoto waishio kwenye mazingira hatarishi na familia katika mazingira maalumu

Siku ya 5

Kuzijengea uwezo jamii,
Ukusanyaji Taarifa na Uwekaji Kumbukumbu

Malengo

- Kuelezea umuhimu wa kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa
- Kujenga stadi za kutayarisha kumbukumbu
- Kujenga stadi katika kudumisha kumbukumbu zinazokidhi mahitaji ya mteja na asasi pamoja na viwango vinavyo hitajika kitaaluma
- Kuelezea na kufafanua kuhusu utetezi na kujenga uwezo
- Kuonyesha kwa vitendo stadi za utetezi na za kujenga uwezo
- Kushirikishana taarifa na uzoefu kuhusu rasilimali zilizopo na stadi za kufanya kazi na watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi

Ukusanyaji Taarifa na Uwekaji Kumbukumbu

Aina Za Ukusanyaji Taarifa

- Taarifa zinazoendelea kuhusu mteja (kwa msimamizi)
- Taarifa za mteja kwa ajili ya asasi kama za Serikali ya kijiji.
- Taarifa binafsi na kumbukumbu

Kwanini Tutunze Kumbukumbu Za Taarifa Za Mteja?

Bungua bongo

Kwanini Tutunze Kumbukumbu Za Taarifa Za Mteja?

- Ili tukumbuke nini kilitokea kwa mteja
- Kuona maendeleo au matatizo ya mtoto na familia
- Kusaidia kujaza dodoso la kukusanyia taarifa zinazohitajika
- Kuweka kazi zetu kwenye maandishi, haswa katika masuala ya ulinzi wa mtoto
- Kuzitumia taarifa tunapowasiliana na wasimamizi au mipango mingine ya huduma

Sifa Za Utunzaji Kumbukumbu Mzuri

Bungua bongo

Sifa Za Utunzaji Kumbukumbu Mzuri

- Za ukweli
- Za kuaminika
- Ukweli utenganishwe na maoni binafsi
  - Zinaonyesha kwa uwazi tathmini ya msaidizi Ustawi wa Jamii na maoni binafsi
  - Zinaonyesha misingi ya tathmini ya msaidizi Ustawi wa Jamii na maoni binafsi
  - Tathmini huweka kumbukumbu za uwezo na mahitaji

Sifa Za Utunzaji Kumbukumbu Mzuri

- Usitumie lugha za kitaalam au lugha za mpito zinazotumika
- Usitumie lugha isiyo sahihi(yenye madhara au inayomkwaza mtu)
- Ujitathmini mwenyewe ili ujiridhishe, ufikirie kuwa mteja anasoma maelezo yako wakati unapoandika

Usiri Wa Kumbukumbu Za Mteja

- Usiri wa taarifa binafsi ni haki ya msingi ya mteja kuhusu huduma za kijamii.
- Usiri wa taarifa za mteja ni taratibu za kitaaluma na katika maeneo mengi kuna wajibu wa kisheria kwa mtoa huduma na Asasi

Usiri…

- Kutotumia majina halisi: Huruhusu matumizi ya taarifa za mteja kwa makusudi maalumu na kwa makusudi ya kitaaluma yanayokubalika ikiwa taarifa za utambulisho zimeondolewa au kuzuiliwa.

Kagle, D.J. (1991). *Social work records, 2nd edition,* Prospect Heights, IL: Waveland

Kanuni 4 Za Usiri Kwa Mteja

- ***Usiri:*** kulinda taarifa binafsi za mteja kwa kutokuziweka wazi(bayana).
- ***Uzuiaji:*** kutoa baadhi ya taarifa zilizo katika kumbukumbu za mteja ambazo ni muhimu katika kumpatia huduma.
- ***Upatikanaji:*** Kumruhusu mteja kufahamu ni taarifa gani zinazokusanywa , na jinsi zinavyo tafsiriwa na matumizi yake

Kushirikishana Taarifa Za Mteja

- Inawezekana kushirikishana taarifa na asasi inapobidi ili kutoa huduma
- Hata hivyo taarifa hazipaswi kushirikishwa ndani ya asasi mpaka kuwe na ulazima wa kufanya hivyo kwa ajili ya kutoa huduma.
- Kushirikishana taarifa nje ya asasi kunahitaji ridhaa ya mteja au mlezi ikiwa mteja ni mtoto.

Kagle, D.J. (1991). *Social work records, 2nd edition*, Prospect Heights, IL: Waveland

Kushirikishana…

- ***Ili kupata "ridhaa toka kwa mteja, maamuzi ya mteja yanapaswa :***
  - Kuwa huru pasipo kutumia nguvu
  - Yaendane na ufahamu kamili kuhusu taarifa gani zinaweza kuwekwa wazi, kwa nani, na kwa makusudi gani.
  - Kuwe na ukomo wa muda
  - Zinazoweza kurejeshwa nyuma(kurejewa)

- Kagle, D.J. (1991). *Social work records, 2nd edition.* Prospect Heights, IL: Waveland

Vigezo Vya Kunukuu Katika Kumbukumbu Za Mteja (Toka Mafunzo Ya Awali Ya Utangulizi Kwa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii)

- Mawasiliano yote yanayofanywa kati ya msaidizi Ustawi wa Jamii na wawakilishi wengine toka katika asasi anayofanyia kazi yanapaswa kurekodiwa kwa haraka iwezekanavyo.
- ***Ni lazima vigezo viwe:***
  - Jina na mtu anaye wasiliana naye.
  - Mahali mawasiliano yalipofanyika
  - Nani alikuwepo
  - Kusudi la mawasiliano
  - Majumuisho kwa ufupi kuhusu yaliyojitokeza wakati wa mawasiliano
  - Ikiwa inamantiki, tathmini ya msaidizi Ustawi wa Jamii kuhusu mawasiliano
  - Matokeo ya mawasiliano ikiwemo makubaliano kuhusu hatua zitakazo fuata
  - Taarifa ni lazima zi sainiwe na kuwekewa tarehe ya mtu anayefanya mawasiliano

Majadiliano Katika Vikundi Vidogo Jinsi Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anavyo Kusanya Taarifa Na Kuweka Kumbukumbu (Dakika 15)

- Mgawanyike katika makundi manne kujadili jinsi gani kumbukumbu zinavyo kusanywa
- Ainisha mambo yale unayohitaji kujifunza
- Onyesha kwa vitendo jinsi ya kukusanya kumbukumbu za mteja

Kujenga Stadi Za Utetezi Na uUwezeshaji

Nini Maana Ya Utetezi?

- Bungua bongo kuhusu dhana
- Aina za Utetezi
- Kanuni

Nini Maana Ya Utetezi?

- Shughuli za Utetezi hutoa msaada unaomwezesha mtu kufahamu ni kwa namna gani anaweza kuzitumia rasilimali za asasi mbalimbali.
- Utetezi vilevile unamaana ya kufanya kazi pamoja na watu wengine ili kubadili mipango au sera katika ngazi ya asasi au jamii.

Utetezi Kwa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii

- Utetezi wa moja kwa moja kwa niaba ya famili:Huwezesha Kupata rasilimali za muda mrefu zinazohitajika kwa ajili ya familia kuwa na uimara toka katika rasilimali za serikali na watu binafsi ndani ya jamii
- Utetezi wenye kuelimisha: Hutoa taarifa kwa familia,majirani, wanarika na watoa huduma wa ndani ya jamii kuhusu mazingira ya familia
- Huwasaidia watu tunaofanyakazi nao kufanya utetezi kwa ajili yao wenyewe.

Nini Maana Ya Utetezi?

- ***Aina za Utetezi***

- Raia;
- Darasa au Kundi
- wanarika
- Vyombo vya Habari
- Hutegemea Tafiti
- Kisheria

Kanuni

- Fanya kwa maslahi bora ya mteja
- Kanya kulingana na matakwa/maelekezo ya mtumiaji
- Mtumiaji awe na taarifa zote
- Toa ushauri kwa uwazi;
- Wateteaji wanapaswa kutambua mipaka yao.
- Ufanye tu kwenyemaeneo ambayo unaujuzi nayo; Endeleza usiri

Kujenga Stadi Za Utetezi Na Uwezeshaji

- Kwa minajili ya mafunzo haya tunaongelea utetezi kwa ajili ya sera ya familia kwa mapana yake ambayo itatoa njia mbalimbali za kinga, tiba, na huduma za msada kwa familia.

Uwezeshwaji?

- Unaonyesha wazo la watu wenyewe kuwa mawakala kwa masuala yao ya kijamii-kisaikolojia na maendeleo ya kiuchumi
- Ni mchakato ambao watu binafsi wanaweza kutengeneza maisha yao wenyewe kwa kupata uwezo wa msingi kama vigezo vya kisaikolojia,mfano kujiamini na wanapopata uwezo kupata rasilimali zinazohitajika ambazo zinawaweka katika kiwango cha kuweza kufanya maamuzi na kuwezesha mikakati ya maisha yenye uchaguzi na vikwazo kwa asasi.

23

Umuhimu Wa Utetezi Na Uwezeshwaji Katika Mchakato Wa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii

- Kwanini utetezi na uwezeshwaji ni muhimu?

Bungua bongo

24

Umuhimu…

- Unapaswa ufanyike ndani ya mazingira ya kijamii,mila na familia halisi ya maisha ya watu.
- Vipo vikwazo vya kijamii,mila, kiuchumi na kisiasa ambavyo vinawanyima watu waishio na VVU na UKIMWI na familia zilizoathirika haki/fursa/ na uwezekano wa kufikia uwezo walionao kwa ukamilifu. Iko haja kwa wataalamu kutoa huduma kwa makundi hatarishi zaidi kwa mazingira ya maambukizi ya VVU.

25

Vigezo Vya Uwezeshwaji

- Upatikanaji wa taarifa
- Kujumuishwa na kushirikishwa
- Uwajibikaji
- Uwezo wa asasi za kijamii

26

Utetezi Wa Jamii

Wasaidizi Ustawi wa Jamii wanapaswa kufanya utetezi kwa ajili ya huduma na msaada kwa kupitia mikutano ya makundi mbalimbali ya kijamii:

- Utetezi katika kamati na mamlaka kwenye ngazi ya kijiji
- Tetea uwakilishi katika ngazi ya taifa na mikutano ya kitaifa na viongozi wenye ushawishi wa misaada na rasilimali kwa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi zaidi. Ushawishi dhidi ya mila zenye athari kama vile usafirishwaji wa watoto, vurugu za masuala ya kujamiiana, unyanyasaji wa kifamilia, kimwili na kingono

NGUVU YA KUMI:
Tusichoweza kukifanya peke yetu tunaweza kukifanya tukiwa na wenzetu

Je Kuna Tofauti Gani Kati Ya Utetezi Wa Jamii Na Utetezi Wa Mtu Binafsi/Familia?

Vitendea kazi vya utetezi:

Je kuna matatizo na fursa?

- Elimu
  - Tabia za mfano
  - Mjadala wa wazi kuhusu unyanyapaa
  - Mafunzo kuhusu unyanyapaa
  - Elimu ya VVU
- ***Kuonyesha mfano***
- Fanya kazi ya malezi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na tegemea kuwa mfano huo utawagusa watu wengine

Vitendea Kazi Utetezi Wa Kijamii

- Kuwafikia viongozi watoa maoni
  - wachungaji
  - Viongozi wa asasi zisizo za kiserikali
  - Viongozi wa kimila na wakijamii
  - Madaktari, wauguzi na maafisa Ustawi wa Jamii
- Utetezi wa wanarika na msaada wa wanarika
  - Wanaoishi na VVU na familia zilizo athirika ni wawakilishi wazuri wa utetezi katika jamii
  - Je unawezaje kuhamasisha vikundi vya wanarika kuongea hadharani?

Utetezi Kuhusu VVU

- Utetezi kuhusu VVU unahusisha kufanya kazi ya kuelimisha jamii kuhusu VVU.
  - VVU sio hukumu ya kifo
  - VVU sio adhabu
  - VVU vinaweza kutibika na kuepukwa kama magonjwa mengine yeyote.
- Msaada wa jamii kuzuia VVU na matibabu huhitaji mjadala wa wazi kuhusu mitazamo ya wazi katika masuala ya kujamiiana na tabia kwani zinaathiri wanaume, wanawake, vijanabalehe na watoto.
- Msaada wa jamii unahitajika katika maeneo yote ya matibabu ikiwemo magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono kama vile kaswende na kisonono

Utetezi Kuhusu VVU

- Msaada wa kijamii unahitajika ili kuelewa uhusiano uliopo kati ya VVU**, *umaskini, kusambaratika kwa familia,*** utumiaji madawa ya kulevya, biashara ya ngono na mada nyinginezo ambazo zinasemekana zimesahaulika au zinaugumu katika kuzijadili kulingana na taratibu za kijamii
- Familia na msaada wa jamii unaweza kuhitajika ili kubadili mitizamo kuhusu uzazi na unyonyeshaji watoto.
- Familia na jamii wanaweza kuhitajika kusaidia hali za kijamii na kiuchumi za watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi zaidi.
- Wasaidizi Ustawi wanapaswa kusaidia watu waishio na VVU na walioathiriwa na VVU kuwa mawakala wa utetezi katika jamii kwa ajili yao binafsi.

Utetezi Unaohusu VVU Hufanyakazi Kazi Vizuri Zaidi Ndani Ya Vikundi

- Wanawake kwa wanawake
- Wanaume kwa Wanaume
  - Je wanapatikana wapi?
  - Kipi ni kigezo kilichozoeleka zaidi?
    - Kwenye baa au kilabuni
    - Michezoni
    - Kanisani na katika Familia
- Vijana kwa vijana
  - Vijana wa kiume na wakike pamoja?
  - Vijana wakubwa wa kiume na wavulana wadogo pamoja?
  - Vijana wakubwa wa kike na wasichana pamoja

Swali La Mjadala

Majadiliano katika vikundi kuhusu njia inayofaa kwa uwezeshwaji katika mazingira ya watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na familia zao nchini Tanzania.

33

Kazi Ya Kikundi

- Zungumzia kuhusu baadhi ya uzoefu wako kuhusu visa vinavyohusu haki za binadamu, maadili au matokeo ya sera
- Fanyeni igizo dhima kwa kutumia mfano wa kisa kimojawapo
- Tengenezeni mpango wa utetezi kwa kisa chenu
  - Andika mambo muhimu (utetezi, haki, sera)
  - Tengeneza angalau hatua mbili za mpango wa utetezi
  - Jadili jinsi utakavyo utekeleza

34

Mfumo Wa Uboreshaji Na Ulinzi Wa Haki Za Mtoto Tanzania

Mfumo wa kitaifa kama ulivyoelezwa katika katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania

Mpangilio Wa Familia Na Jamii

- Wakati mikataba ya kimataifa kuhusu watoto na katiba ya jamhuri ya muungano inamuangalia mtoto kama suala la haki na inahitaji nchi/serikali kumchukulia mtoto hivyo, kiutendaji jambo hili halishirikishwi katika familia. Idadi kubwa ya familia na jamii katika nchi humchukulia mtoto kama kitu cha ulinzi, rasilimali kwa yote, kazi na jukumu lao la kuhakikisha ukoo unaendelezwa

Kanuni Sita:
Suala Kubwa La Malezi Na Ulinzi Wa Watoto Na Haki

1. Tambua ni kwa kiasi gani jamii ya kimataifa inaweza kuhusishwa wakiwa ni wadau katika juhudi na kujaribu kuhamasisha ushirikiano
2. Tambua umuhimu wa kushirikishana uzoefu muhimu katika ngazi ya Taifa na jamii.

Kanuni Sita…

3. Anza na mtazamo wenye uhalisia kuhusu jambo gani linaweza kufikiwa na katika muda gani. Mtazamo wa jinsi hiyo unajaribu kutengeneza sera na utaratibu unaozingatia muda wa utekelezaji. Malengo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.
4. Anzisha mfumo wa ufuatiliaji ili kuwezesha upatikanaji wa mrejesho na mipango zaidi.

Kanuni Sita…

5. Katika kutengeneza mipango, tumia utaratibu wa kuhusisha sekta mbalimbali na kutambua umuhimu wa jukumu ambalo asasi inatekeleza katika kuendeleza maslahi ya mtoto na utekelezaji wa mipango hiyo ili kuhakikisha mchango binafsi (i.e. ujuzi na ushiriki wao)

Kanuni Sita…

6. Husisha familia, jamii na uongozi wa ngazi ya wilaya
   Katika kupanga na kutekeleza mipango hiyo ili kuhakikisha mchango wa mtu binafsi (i.eujuzi na ushiriki wao) na msaada wao. Kwa maneno mengine, kanuni hii inatambua kuwa familia na jamii ni sehemu ya ulimwengu wa jamii ya mtoto ni muhimu kupata matumaini yao na msaada ili kuendelea mbele.

Kujenga Ufahamu Mkubwa Kuhusu Haki Katika Jamii

- Umuhimu wa kuhamasisha unatambulika kwa azimio lamtoto (kifungu 42: vyama katika nchi vina jukumu la “kuzifanya kanuni na maeneo ya utoaji vitu kwa siku za mbele kufahamika kwa upana, na kwa njia sahihi zinazotumika, kwa watu wazima na watoto vilevile” Kwa upande mwingine, wafanyakazi wengi wa jamii kama vile vyombo vya sheria, maafisa wa polisi, maafisa ustawi wa jamii, madaktari na waalimu wa shule pengine hawana ufahamu kabisa au wanaufahamu usiofaa kuhusu haki za watoto.

Kujenga Ufahamu Mkubwa Kuhusu Haki Katika Jamii

- Kuziwezesha familia na jamii
- Mchakato ni lazima uanze kwa kuangalia muundo wa familia kuangalia mgawanyo wa uwezo wa kufanya maamuzi na jinsi rasilimali za familia na majukumu ya familia yalivyo gawanywa.
- Kutoa huduma za ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa watoto na kutojaliwa katika ngazi ya jamii.

Kujenga Ufahamu Mkubwa Kuhusu Haki Katika Jamii

- Kuzifanya asasi za kijamii na kisheria katika ngazi ya jamii kutoa huduma kwa makundi ya watu wenye fursa finyu kama masikini, na watoto wasio na uwezo. Kuongeza ufahamu wa wanajamii kuhusu ulinzi wa mtoto, haki, kushughulukia unyanyasaji –na jinsi ya kusaidia.
- Kutoa ufahamu kuhusu majukumu na wajibu wa asasi za kijamii m.f. familia, majirani kuhusu ulinzi wa mtoto.
- Familia na asasi za msingi kuendelea na taratibu za kimila zenye wigo mpana katika ulinzi wa mtoto.

Kujenga Ufahamu Mkubwa Kuhusu Haki Katika Jamii

- Familia na asasi zingine za msingi za malezi na huduma kwa mtoto zinapaswa kutambua haki za mtoto katika mazingira yao.
- Njia nyingine za malezi ya watoto katika jamii za kiafrika.
- Kujenga uelewa wa kutambua njia hizo na kuwa na njia mbadala zisizo na unyanyasaji katika malezi Ya familia.

Kufanya Kazi Na Vikundi, Matukio Ya Kijamii, Vyombo Vya Habari, Waelimishaji Rika.

Je Kuna Vikundi Vya Aina Gani Katika Vijiji/Jamii Mlizotoka Ambavyo Vinaweza Kuwa Na Manufaa Kwa Mtoto Na Familia Unazofanya Kazi Nazo?

Bungua bongo

Je Kuna Vikundi Vya Aina Gani Katika Vijiji/Jamii Mlizotoka Ambavyo Vinaweza Kuwa Na Manufaa Kwa Mtoto Na Familia Unazofanya Kazi Nazo?

- Vikundi vya malezi na huduma vinavyowasaidia watoto.
- Kamati za maendeleo katika serikali za mitaa.
  - Watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi
  - Nyinginezo?
- Je kuna vikundi vinavyohusiana na masuala ya VVU?
  - Vikundi vya kusaidiana
  - Kamati za kijamii zinazoshughulikia vikundi vinavyojihusisha na masuala ya UKIMWI
  - Vikundi vya wazazi, vikundi vya kidini, vikundi vya vijana n.k.
- Vikundi vya wanawake, vikundi vya wazazi.
- Vikundi vya kidini na vinginevyo.

Kufanyakazi Na Vikundi, Matukio Ya Kijamii, Vyombo Vya Habari, Waelimishaji Rika.

- Kutumia vikundi vya wanarika:
- Vikundi vyenye jinsi moja
- Vikundi vyenye jinsi tofauti
- mafunzo ya uongozi katika vikundi vya wanarika: kufundisha stadi za maisha.

Kufanya Kazi Za Matukio Ya Kijamii,

- Matukio ya kimila ndani ya jamii yanaweza kutumika kama mikusanyiko ya kuendesha kampeni dhidi ya unyanyasaji wa watoto. m.f. sherehe za jando kwa vijana wa kiume, unyago kwa watoto wa kike, Sherehe za mwaka mpya, sherehe za mavuno ya mwaka, sherehe za kidini n.k.
- Je unaweza kufikiria mifano mingine au ni kwa jinsi gani mifano hii yaweza kuwa yenye manufaa katika kupeleka ujumbe kuhusu ulinzi wa mtoto

Kufanya Hazi Na Vyombo Vya Habari

- Je ni ipi mifano ya vyombo vya habari vya kijamii?

Bungua bongo

Kufanya Kazi Na Vyombo Vya Habari

- ***Mifano ya vyombo vya habari ndani ya jamii:***
- vituo vya radio vilivyo ndani ya jamii, magazeti, waandishi wa habari, Luninga?
- Unaweza pia kufanya kazi na waimbaji, wacheza muziki, wengine mnaoweza kushirikishana taarifa
- Kutengeneza ujumbe juu ya kukinga: maneno yenye vina, wito,Michezo na mikutano yakijiji
- Kutengeneza ujumbe jinsi ya kutoa taarifa zinazohusu maswala ya watoto waishio katika mazingira hatarishi na kuwaunganisha na huduma
- Kushirikishana taarifa kuhusu rasilimali za msaada zilizopo Kuhusu maswala ya haki za mtoto na ulinzi.
- Mbinu za utoaji taarifa matukio ya unyanyasaji wa mtoto ndani ya jamii.vijijini

Kufanya Kazi Na Jamii Vijijini Kipindi Cha Kushirikishana

- Waeleze wana kikundi washirikishane uzoefu kuhusu yale waliyofanya katika kufanyakazi na jamii vijijini.
- Je kuna shughuli maalumu ambazo zinaonyesha mafanikio?
- Je ni shughuli gani zenye mafanikio zinazoweza kusimuliwa?
- Kuna masuala gani tunayohitaji kuyashughulikia?

Maonesho ya Rasilimali

Kesi Menejimenti Kushirikishana Rasilimali

Jadili:

- Ni zipi rasilimali zinazoweza kusaidia familia?
- Je? Familia zinawezaje kuhusishwa katika kusaidia wengine?
- Je tunawezaje kupata msaada wa kiuchumi kwa ajili ya familia zenye uhitaji?
- Je ni rasilimali gani zinazoweza kusaidia mahitaji kwa maendeleo na ulinzi wa mtoto?

Kutengeneza Orodha Ya Rasilimali Kwa Ajili Ya Msaidizi Ustawi Wa Jamii

- Kumbuka ramani za kutambua rasilimali tulizotengeneza katika mafunzo ya utangulizi kwa wasaidizi Ustawi wa Jamii(PSWI)
  Jadili
- Je tunaweza kutengeneza orodha ya rasilimali ambazo tumeona kuwa zinaweza kutumika katika kuwasaidia watoto?
  - Tumia dakika moja kutengeneza orodha yako mwenyewe.
  - Ili Kuzishika rasilimali tunazoshirikishana (Tumia mpira—Urushe kwa washiriki wanaoshirikishana rasilimali na endelea kurushiana na wengine)

Mpango Wa Kupima Uelewa
(Jaza Dodoso La Mwisho Wa Mafunzo)

Sherehe Za Ufungaji Mafunzo Na Kushehereka

Kwa Sasa Sisi Ni Wasaidizi
Ustawi Wa Jamii Kamili